MWITO PROG **1088** KISWAHILI SCRIPT

TRANSWORLD RADIO (TWR)

SCRIPTURE ROMANS-: 5:12

INTRO:

Nakukaribisha tena msikilizaji wangu kwa kipindi cha MWITO nambari 1087 kutoka studio zetu za Nairobi.Sina shaka kwamba Mungu amekulinda na hata kukufikisha siku ya leo ambapo tunakutana tena.Nakukumbusha kuwa kipindi hiki kinakujia kwa hisani na udhamini wa huduma ya kimataifa ya Macedonian Call yake Harod Williams.Ikiwa ungependa kujipatia nakala ya agano jipya la Bibilia bila malipo baki nami hadi mwisho wa kipindi hiki nitakujulisha jinsi ya kuipata.

Leo tunendelea tunendelea na somo letu na linatoka sura ya 5 ya Warumi.Kwenye kipindi kilichopita nambari 1087 tulisoma aya ya 11 na Nitawakumbusha ilikuwa inasemaje ,kisha tutaendelea**……**11… ***Wala si hivyo tu ila pia twajifurahisha katika Mungu kwa Bwana wetu Yesu Kristo,ambaye kwa yeye sasa tumeupokea huo upatanisho.***

Naam mpendwa upatanisho ni athari ya kifo cha Kristo.Tumepokea neema kutokana na upatanisho huo.Na leo tutasoma aya ya 12.Athari ya dhambi iliotuzonga na suluhisho lake.Ukamilifu wake uko kwenye athari saba za matokeo ya utakaso ambazo tulizungumzia kwenye vipindi vya hivi punde.Vilikuwa kwenye aya ya 1 hadi ya 11.Sasa tunamwona binadamu ambaye alikakanyika alipokumbwa na dhambi tangu enzi ya bustani ya edeni.Jinsi joka alivyomdanganya mwanamke hadi alipokula tunda toka mti uliokatazwa.Mwanamke alidanganyika,lakini adamu hakudanganyika alililichukua lile tunda kwa hiari yake na kulila.Kutokana na tendo hilo kiwango chake cha dhambi kilikuwa hata kikubwa zaidi.Kitendo hicho kilimfanya adamu akafa kifo cha kiroho.Jinsi Mungu alivyokuwa ameoya kwamba atakayelila tunda kutoka mti huo kwa hakika atakufa.Kutokana na kifo hicho cha kiroho,uhusiano kati ya Munu na binadamu ulikatika.Kifo hiho kilikuwa cha kiroho ,japo waliendelea kuishi kimwili,lakini kiroho walikuwa wamekufa.Hata hivho walitengwa na Mungu kutokana na dhambi hiyo.Neno kifo linamaanisha utenganisho.Na hiyo ndiyo maana tunasema mtu anapokufa kwamba ametenganishwa nasi.Yaani uhai umetoka kwenye mwili.Mwili hurudi mchangani ulikotoka nayo roho humrudia muumba wake.Jambo la kutisha ni kwamba kunao wanaokufa vifo vya kiroho na kimwili.Wale ambao hawakuwahi kumpokea kristo kuwa mwokozi wao.Yaani walikufa kwenye dhambi.Maandiko yanasema kuwa adamu alikufa kiroho baada ya kula lile tunda.Na kutokana na kitendo hicho

dhambi iliingia duniani.Binadamu aliingiwa na dhambi ikasababisha kifo..Adamu alipokufa kifo hicho kilifwata uzao wake.Mimi na wewe tulikuwa tuliathirika na dhambi hiyo kwa kuwa tulitokana na uzao wa adamu.Tangu wakati huo kila binadamu aliyezaliwa alikuwa na dhambi za uzao wa adamu.Dhambi ya urithi kutoka uzao wa adamu.Ndiposa maandiko yanasema kila mtu ametenda dhambi na adhabu yake ni kifo,isipokuwa mtu atubu dhambi zake na kuoshwa na damu ya Yesu Kristo.Yaani sote tumetenda dhambi na kupungukiwa na utukufu wa Mungu.***Aya ya 13 inasema kwamba maana kabl ya sheria dhambi ilikuwamo ulimwenguni,lakini dhambi haihesabiwi isipokuwepo sheria,walakini mauti ilitawala tangu Adamu mpaka Musa nayo ilitawala hata wasiofanya dhambi ifananayo na kosa la adamu,aliye***